Washington State Department of Social & Health Services
Transforming lives

Ruzuku zako za Fedha Taslimu au Chakula za DSHS

Your DSHS Cash or Food Benefits

JINA LA MTEJA (MKUU WA KAYA)

NAMBARI YA UTAMBULISHO WA MTEJA:

Ruzuku za Fedha taslimu za DSHS TANF, Msaada wa Fedha taslimu wa Wakimbizi, Fedha taslimu za ABD, Ubadilishaji Fedha

☐ **Dhumuni**

DSHS hutoa ruzuku za fedha taslimu kwa wakazi wenye kipato cha chini wanaostahili kupata programu za usaidizi wa umma.

Ruzuku hizi husaidia kulipia gharama za msingi za maisha (RCW 74.04.770).

Ruzuku za fedha taslimu za TANF zinapaswa kutumiwa tu kwa faida ya watoto unaowatunza. Tunaweza kuhitaji uthibitisho kwamba unatumia ruzuku yako ya TANF kwa mahitaji ya watoto (RCW 74.12.260).

☐ **Matumizi Yanayofaa**

Unaweza kutumia ruzuku yako ya fedha taslimu kwa ajili ya gharama za maisha kama vile:

- Hifadhi
- Chanzo cha Nishati
- Chakula
- Usafiri
- Nguo
- Ukarabati wa nyumba
- Usafi wa kibinafsi
- Gharama za ajira

☐ **Matumizi Haramu**

Chini ya RCW 74.08.580, hairuhusiwi kisheria kutumia kadi za Uhamisho wa Ruzuku za Kielektroniki (EBT) au fedha taslimu kutoka kwenye kadi za EBT kwa ajili ya:

- Kamari. Kamari ni pamoja na tikiti za bahati nasibu, pull tabs, punch boards, bingo, mbio za farasi, michezo ya kasino, na mchezo wowote wa bahati nasibu unaopatikana katika RCW 9.46, 67.16, na 67.70.
- Kununua huduma katika maduka ya kuchora tatoo, kutoboa mwili, au sanaa ya mwili.
- Kununua sigara au tumbaku.
- Kununua bidhaa zenye kulevya.
- Kununua bidhaa au huduma katika:
  - Klabu za pumbe.
  - Maduka ya bia au divai isipokuwa yakidhinishwa kama muuzaji wa SNAP au WIC.
  - Klabu za usiku.
  - Mashirika ya dhamana.
  - Makampuni ya kamari.
  - Kumbi za burudani za watu wazima zenye maonyesho ya ngono.
  - Mahali popote ambapo mtu aliye chini ya umri wa miaka 18 haruhusiwi
    - Kwa mfano, wauzaji wa bangi ambapo bidhaa za bangi na/au bangi zinauzwa.

Ruzuku za Chakula za DSHS

☐ **Dhumuni**

Programu za msaada wa chakula za DSHS ni pamoja na:

- Chakula cha Msingi.
- Programu ya Msaada wa Chakula kwa ajili ya wahamiaji halali (FAP).
- Mradi wa Maombi ya Pamoja wa Washington (WASHCAP).
- Msaada wa Chakula wa Mpito (TFA).

Programu hizi hutoa msaada kwa watu wenye kipato cha chini kuweza kununua chakula kwa kutumia kadi za kielektroniki za uhamishaji wa mafao (EBT).

☐ **Matumizi Yanayofaa**

Wewe, na familia yako, mnaweza kutumia ruzuku zenu za chakula kununua chakula kutoka kwa muuzaji aliyeidhinishwa na USDA, Huduma ya Chakula na Lishe (FNS).

Unaweza kutumia ruzuku zako kununua:

- Mikate na nafaka.
- Matunda na mboga mboga.
- Jibini, maziwa, na bidhaa za maziwa.
- Nyama, samaki, kuku, na mayai.
- Vyakula vingi zaidi ya vyakula vya moto ambavyo tayari vimeandaliwa.
- Mbegu na mimea ambayo huzalisha chakula.

☐ **Matumizi Haramu**

Ni kinyume cha sheria:

- Kutumia ruzuku za chakula kwa kitu kingine chochote isipokuwa kununua chakula kwa ajili ya wanafamilia wanaostahiki.
- Kuuza, au kujaribu kuuza, kadi yako ya EBT.
- Kubadilisha ruzuku zako, au chakula kilichonunuliwa kwa kadi yako ya EBT, kwa kitu kingine chochote cha thamani (biashara haramu).

  Mifano ya biashara haramu ni pamoja na kubadilishana ruzuku za chakula kwa fedha taslimu, dawa za kulevya, au silaha.
- Kumpa ruzuku zako mtu yeyote ambaye hayupo katika kaya yako.
- Kutumia ruzuku za chakula ili kununua vitu visivyokua chakula. Mifano ni pamoja na sigara, tumbaku, bia, divai, pombe, vifaa vya nyumbani, sabuni, bidhaa za karatasi, vitamini, dawa, au chakula cha wanyama rafiki.
- Kutumia ruzuku zako za chakula kulipia akaunti za mkopo.

Barcode label

14520

Ruzuku za Fedha taslimu za DSHS TANF, Msaada wa Fedha taslimu wa Wakimbizi, Fedha taslimu za PWA, ABD, Ubadilishaji Fedha	Ruzuku za Chakula za DSHS
☐ **Adhabu ya Matumizi Haramu** Ikiwa utatumia kadi yako ya EBT au fedha taslimu kutoka kwenye kadi yako ya EBT kinyume cha sheria au isivyofaa, tunaweza: • Kuteua mpokeaji atakaelinda ili kusimamia ruzuku yako ya fedha taslimu. • Kutaka uthibitisho kwamba unatumia ruzuku yako kwa ajili ya watoto unaowatunza. • Kukatisha ruzuku zako za fedha taslimu. • Kukuchukulia hatua za kisheria, ikiwa ni pamoja na mashtaka ya jinai. ☐ **Ada za mashine ya kutoa pesa kiotomatiki (ATM) kwa ajili ya Utoaji fedha wa EBT** Unapotumia kadi yako ya EBT kutoa pesa taslimu kwenye ATM: • Mmiliki wa ATM au benki inayoendesha mashine hiyo wanaweza kutoza ada ya ziada. • Idara hailipi au kufidia ada za ziada za ATM. • Unaweza kurudishiwa pesa kutoka kwa baadhi ya maduka bila ada.	☐ **Adhabu ya Matumizi Haramu** Ikiwa utatumia vibaya kwa makusudi ruzuku zako za chakula, unaweza: • Kuhitajika kulipa ruzuku zozote za biashara haramu. • Kufutiwa ustahiki na kupoteza ruzuku zako: o Kwa angalau mwaka mmoja. o Hadi milele. o Kufutiwa ustahiki hata kama utahamia jimbo lingine. • Kukabiliwa na faini. • Kukabiliwa na hatua za kisheria, ikiwa ni pamoja na mashtaka ya jinai. DSHS itashirikiana na mamlaka za jimbo, za eneo, na serikali kuu ili kushtaki biashara haramu ya ruzuku za chakula.

Kwa kusaini hapo chini, nakubali kwamba matumizi yanoyofaa na ya kisheria ya ruzuku za fedha taslimu na chakula za DSHS yamefafanuliwa. Naelewa matumizi yanayofaa ya ruzuku na adhabu kwa matumizi haramu. Naelewa ustahiki wangu wa kupata ruzuku za DSHS hautaathirika ikiwa sitasaini fomu hii. Mtu yoyote atakaeshindwa kusaini fomu hii bado anakabiliwa na adhabu ya programu au jinai kwa matumizi haramu ya ruzuku.

Naelewa kadi yangu ya EBT inatoa historia ya miamala yangu kwa DSHS, ikiwa ni pamoja na mahali ninapotumia kadi yangu. Naelewa DSHS itatumia taarifa hii, na historia yangu ya maombi ya kubadilisha kadi, kuchunguza matumizi mabaya ya ruzuku za fedha taslimu au ruzuku za chakula.

SAINI YA MWOMBAJI	TAREHE

☐ Amekataa kusaini; Herufi ya Kwanza ya Jina la Mfanyakazi wa DSHS _____